

KUMSAIDIA MTOTO WAKO KUWA TAYARI KUSOMA

NEWCOMER
PARENT
RESOURCE
SERIES

Wewe ndiye mwalimu mkuu wa mtoto wako. Kila siku, anakutazama, anakusikiliza na kujifunza kutokana na mfano wako. Wewe pia ndiye chanzo muhimu zaidi cha usaidizi kwa mtoto wako—na kwa kuwa watoto hufanya vyema wanapokuwa katika mazingira mazuri ambapo wanahisi salama, wanaheshimika na kupendwa—unavyowajali itakuwa na matokeo makubwa kwa jinsi wanavyosoma.

Hapa kuna mambo saba muhimu unayoweza kufanya kumsaidia mtoto wako kusoma:

1. WAPENDE.

Kuwa mzuri na mwenye upendo kwa mtoto wako. Onyesho upendo wako kwa kumtazama, kujibu vizuri ishara zake na kumsaidia anapokuhitaji. Kuwa na matumaini na umsaidie mtoto wako kuhisi kwamba ni wa maana na muhimu.

2. WASIKILIZE NA ONGEA NAO.

Unapongea na mtoto wako, mpe muda wako wote. Hii itamsaidia kujifunza jinsi ya kuwasiliana na wewe na wengine. Kusimulia hadithi, kuimba, kukariri na kusoma pamoja huboresha pia ujuzi wake wa kusoma na kusikiliza.

3. CHEZA, CHEZA, NA UCHEZE ZAIDI.

Unapochukua muda ukicheza na mtoto wako unatia moyo ukuaji na maendeleo yake. Tambua anachopenda kucheza, jiunge na furaha na mjaribu mambo mapya pamoja. Unaweza pia kumpeleka mtoto wako kucheza na vikundi na mipango ya familia ili kumsaidia kuzoea kucheza na watoto wengine.

4. TAFUTA MUDA WA SHUGHULI YA KUCHEZA KILA SIKU.

Watoto wadogo wanahitaji kushughulika kila siku. Kukimbia, usawazisho na kupanda jengo ili kupata mifupa na misuli yenye nguvu, kukuza ujuzi na kuboresha afya na furaha kwa ujumla.



5. HIMIZA KULA VIZURI.

Mtoto wako anahitaji vyakula vizuri na mitindo mizuri ya kula ili kuwa mwenye nguvu na afya. Lishe nzuri humpa mtoto wako nguvu ya kusoma, kucheza na kukua. Kaa na mtoto wako anapokula mara kadhaa kwa siku. Huu pia ni wakati mzuri wa kutangamana.

6. UNDA RATIBA YA KILA SIKU.

Ratiba zinaweza kuwasaidia watoto kuhisi salama zaidi. Zinaweza pia kupunguza tabia ngumu na kuongeza kujitegemea. Kuwa na ratiba ya kila siku ya kuamka, kufua, kwenda choo, kuvaa, kula vyakula na vitafunio, kwenda kitandani na kucheza (sana na kwa utulivu). Wakati mwingine, ratiba za mpango au shule zinahitaji kubadilishwa ili kumsaidia mtoto ambaye ana mahitaji maalum. Kwa mfano, baadhi ya watoto wanahitaji msaada au muda zaidi kutumia choo au kutulia ili kulala.

7. HAKIKISHA MTOTO WAKO ANAFANYIWA UCHUNGUZI WA AFYA NA WA KUKUA MARA KWA MARA.

Watoto wanasoma vizuri wakihisi vizuri, wakisikia na kuona vizuri, na wakila vyakula vizuri. Uchunguzi wa afya na chanjo husaidia kumweka mtoto wako mwenye afya. Ikiwa una wasiwasi kuhusu maendeleo ya mtoto wako au jinsi anavyofanya kwenye mpango unaweza pia kuongea na wahudumu wa mpango.

Imechukuliwa na kibali kutoka kwa Best Start Resource Centre.

Tembelea cmascanada.ca/cnc/parents kwa maelezo zaidi ya lugha mbalimbali ya wazazi



SUPPORTING CHILD CARE IN THE SETTLEMENT COMMUNITY / SOUTIEN DE LA GARDE DES ENFANTS DANS LA COMMUNAUTÉ DE RÈGLEMENT
Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada / Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada